**HOTUBA YA MKUU WA MKOA MHE. MBONI MHITA KATIKA KONGAMANO LA WAFANYABIASHARA NDOGONDOGO MKOA WA SHINYANGA LINALOFANYIKA TAREHE 22 AGOSTI, 2025**

- ***Mwenyekiti wa CCM Mkoa,***
- ***Katibu CCM wa Mkoa,***
- ***Katibu Tawala wa Mkoa,***
- ***Wajumbe wa Kamati ya Usalama ya Mkoa,***
- ***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,***
- ***Wakuu wa Sehemu na Vitengo kutoka Sekretarieti ya Mkoa,***
- ***Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa,***
- ***Wakuu wa Taasisi (VETA, SIDO, NSSF na NMB)***
- ***Viongozi wa Dini,***
- ***Viongozi wa wafanyabiashara ndogondogo,***
- ***Wafanyabiashara ndogondogo (****bodaboda, machinga, wasusi, wauza mbogamboga na matunda, seremala, mamalishe na baba lishe****)***
- ***Waandishi wa Habari,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia sisi sote afya njema na kutufikisha mahali hapa salama. Nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu Tawala wa Mkoa na timu yake kwa maandalizi mazuri ya kongamano hili.

***Ndugu Washiriki,***

Tarehe 25 Januari, 2022 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya mazungumzo na uongozi wa wafanyabiashara ndogondogo Jijini Dar es Salaam. Katika mazungumzo hayo alibainisha dhamira ya Serikali kuwatambua wafanyabiashara ndogondogo nchini kama kundi maalum linalohitaji uratibu na usimamizi wa karibu.

***Ndugu Washiriki,***

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Shinyanga una jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 28,111 ambapo kati yao wanaume ni 13,211 na wanawake ni 14,900. Hivyo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inaendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya uendeshaji wa shughuli za kiuchumi kwa wafanyabiashara ndogondogo kulingana na makundi yao ili kuwawezesha kufikia malengo ya kuwa wafanyabiashara wa kati na wakubwa. Baadhi ya jitihada hizo ni pamoja na:-

1. Kusimamia na kuratibu zoezi la kuwatambua, kuwasajili na kuwapatia vitambulisho vya kidijitali vya ujasiriamali wafanyabiashara ndogondogo katika Halmashauri zote sita. Vitambulisho hivi ni moja ya fursa kubwa ya kiuchumi ambayo imewezeshwa na Serikali kwa kuwa kitambulisho hicho kinamwezesha mfanyabishara ndogondogo kuwa na sifa ya kunufaika na mkopo wa riba nafuu ya asilimia 7 unaotolewa na Serikali kupitia benki ya NMB.

   Hadi kufikia tarehe 31 Julai, 2025 jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 2,181 wamesajili.

2. Kutengeneza mazingira wezeshi ya upatikanajia wa mitaji kwa wafanyabiashara ndogondogo kupitia Mkopo wa asilimia 10 unatokana na mapato ya ndani ya Halmashauri ambapo mkopo huo hutolewa kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya shilingi Billioni 4.9 kimetolewa ambao kiasi cha shilingi Bilioni 2.6 kimenufaisha vikundi 256 vya wanawake, kiasi cha shilingi Bilioni 2.2 kimenufaisha vikundi 153 vya Vijana na kiasi cha shilingi millioni 150.8 kimenufaisha vikundi 24 vya Watu wenye Ulemavu. Uratibu wa utoaji wa mkopo huu kutoka katika Halmashauri zote unaendelea hivyo niwahamasishe wafanyabiashara ndogondogo wote kujiunga katika vikundi ili kupata sifa ya kunufaika na mkopo huu nafuu usio na riba.

3. Kuwapanga wafanyabiashara ndogondogo katika maeneo rasmi yaliyotengwa na kuendelezwa.

   Mkoa umefanikiwa kutenga jumla ya maeneo 16 kwa ajili ya kuwezesha wafanyabiashara wadogo kutekeleza shughuli za biashara na viwanda vidogo.

   i. Halmashauri ya Kahama Manispaa imetenga eneo la Zongomela;
   ii. Halmashauri ya Ushetu maeneo 08 ya Uyogo, Ididi, Ufaransa, Mwadui, Shilabela, Bugomba A, Mseki na Kengeme;
   iii. Halmashauri Manispaa ya Shinyanga maeneo matatu (03) ya Soko la Ibinzamata, Soko la Wamachinga Mnara wa Voda na Soko la Mitumba la Ngokolo;
   iv. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga maneo manne (04) ya Ishina – Bulandi na Iselamagazi

v. Halmashauri ya Kishapu eneo moja (01) soko la Wajasiriamali la Swalala - Mhunze.

Aidha, Mkoa umesimamia uanzishwaji wa Vituo Jumuishi vitatu (3) vilivyopo katika Halmashauri za Kahama (Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi cha Nyihogo); Kituo cha Uwezeshaji, Urasimishaji na Uendelezaji wa Biashara kilichopo katika Manispaa ya Shinyanga na Ofisi Ndogo ya Biashara iliyopo eneola

Maganzo katika Halmashauri ya Kishapu. Serikali ya Mkoa inaendelea kufanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha Taasisi muhimu ikiwemo TRA, SIDO, Ardhi na nyinginezo zinaendelea kutoa huduma katika vituo Jumuishi.

4. Kuratibu na kusimamia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya masoko kwenye Halmashauri.

   Mkoa wa Shinyanga una jumla ya masoko 86 ikijumuisha masoko makubwa 8, Masoko ya Kati 22 na masoko madogo 56. Aidha, Mkoa wa Shinyanga una jumla ya magulio 18.

   Ikiwa ni juhudi ya kuboresha hali ya masoko katika mkoa, Serikali imejenga masoko mapya ikiwemo soko la wajasiriamali la Ibinzamata, soko la mitumba lililopo eneo la Ngokolo na Soko la Machinga la Mnara wa Voda yaliyopo katika Manispaa ya Shinyanga. Vilevile, miundombinu ya masoko ya Namanga na Sango yaliyopo manispaa ya Kahama imeboreshwa na kuwa katika hali nzuri na kuridhisha.

5. Kuhakikisha kundi la wafanyabiashara ndogondogo linakuwa na uongozi kuanzia ngazi ya Masoko, Halmashauri na Mkoa ili kuwajengea uwezo

katika masuala ya uongozi bora, ujasiriamali, mawasiliano na uzingatiaji wa Katiba ya nchi.

Serikali imetoa kiasi cha shilingi million 50 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi itakayotumiwa na viongozi wa wafanyabiashara ndogondogo. Ofisi hii imejengwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga na kwa sasa ipo katika hatua ya ukamilishaji. Tunatarajia hadi kufikia 31 Septemba, 2025 Ofisi hii itakuwa imekamilika na kukabidhiwa kwa viongozi kw ajili ya kuendelea kuitumia.

Pamoja na ujenzi wa Ofisi hiyo ya Mkoa, pia Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu imefanikiwa kujenga Ofisi ya Wafanyabiashara ndogondogo itakayotumiwa na viongozi wa ngazi ya Halmashauri. Ofisi hiyo imejengwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani ambapo jumla ya shilingi milioni 46.6 zimetumika kukamilisha ujenzi.

Nitoe rai kwa Halmashauri zote zilizobaki kutenga fedha za ujenzi wa Ofisi za wafanyabiashara ndogondogo maarufu kama Ofisi za Machinga ili kuboresha mazingira ya ufanyajikazi.

***Ndugu Washiriki,***

Mkoa unatambua umuhimu mkubwa wa sekta ya wafanyabiashara ndogondogo katika kukuza Uchumi na kuinua maendeleo ya mtu mmoja, Mkoa na Taifa kwa ujumla. Nikiri kuwa sekta ya wafanyabiashara ndogondogo inachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa Uchumi. Hivvyo kutokana na umuhimu huu, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itaendelea kuratibu kwa karibu shughuli zote za uwezeshaji wa wafanyabishara ndogondogo ili kuhakikisha mazingira yanaendelea kuwa bora.

***Ndugu Washiriki,***

Naomba pia nitumie kongamano hili kuwakumbusha kuwa mwaka huu ni mwaka muhimu sana kwa Taifa kwa kuwa ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu ambapo tutamchagua Rais wa Nchi, Wabunge na Madiwani. Nitoe rai kwenu kwanza kuhakikisha mnaitunza amani ya Nchi kwa kuendelea kufanya shughuli zenu za kiuchumi bila kuvunja sheria za Nchi. Pili niwakumbushe kuwa kupiga kura ni wajibu wa kila mwananchi mwenye umri kuanzia miaka 18 hivyo itakapofika siku ya uchaguzi tujitokeze kwa wingi kutumia haki hiyo ya kikatiba.

**Mwisho**, niwashukuru wote kwa kushiriki kikamilifu katika kongamano hili na kwa mjadala mzuri ambao utatuwezesha kuboresha zaidi huduma.

***Asanteni sana kwa kunisikiliza.***

***"JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA"***